# Agano Langu la Ubatizo

Agano ni ahadi tunayofanya na Baba wa Mbinguni. Soma kuhusu vitu vitatu tunavyoahidi kufanya tunapobatizwa. Kisha andika kuhusu kile unachoweza kufanya ili kushika agano lako la ubatizo.

## Daima Kumkumbuka Yesu Kristo



Wakati Elena alipowaona wengine wakimtendea mabaya mtu fulani, alifikiria kile ambacho Yesu angefanya.

Je, ninawezaje kumkumbuka Yesu:

*"Daima kumkumbuka yeye" (Moroni 4:3).*

## Kushika Amri Zake



James alichagua kutoangalia video zilizo na maneno na picha mbaya.

Amri Ninayoweza kushika:

*"Kushika Amri Zake" (Moroni 4:3).*

## Jichukulie Jina Lake Juu Yako

Nana alimwambia rafiki yake kwamba yeye ni wa Kanisa la Yesu Kristo la Watakatifu wa Siku za Mwisho.

Kile ambacho kujichukulia jina Lake juu yetu humaanisha kwangu:

*"Jichukulie juu [yako] jina la [Yesu Kristo]" (Moroni 4:3).*





## KUSHIKA AGANO LANGU

Hapa kuna baadhi ya njia za kushika agano lako la ubatizo.

### Wasaidie Watu



Akio alimsaidia mdogo wake kazi yake ya nyumbani ya hisabati.

Nani ninaweza kumsaidia:

*"Kubebeana mizigo, ili ipate kuwa miepesi" (Mosia 18:8).*

### Tubu Unapofanya Kosa



Baada ya Isa kusema kitu kibaya kwa dada yake, aliomba kwa Baba wa Mbinguni. Kisha alimuomba dada yake amsamehe.

Jinsi gani ninaweza kutubu:

*"Watubu na kuzaliwa tena" (Alma 5:49).*

### Wafariji Wengine



Lucas alimtembelea rafiki yake ambaye babu yake amefariki.

Jinsi gani ninaweza kumfariji mtu:

*"Kufariji wale ambao wanahitaji kufarijiwa" (Mosia 18:9).*

VIELELEZO NA KELLY SMITH

### UTHIBITISHO WAKO

Baada ya ubatizo mwenye ukuhani ataweka mikono yake juu ya kichwa chako.

Atakuthibitisha wewe kuwa muumini wa Kanisa la Yesu Kristo la Watakatifu wa Siku za Mwisho na kukubariki ili upokee kipawa cha Roho Mtakatifu (ona Mafundisho na Maagano 33:15).

### KILE BABA WA MBINGUNI ANACHOKUAHIDI WEWE

Wakati tunapobatizwa na kuthibitishwa, Baba wa Mbinguni anatuahidi kwamba daima Roho Wake atakuwa pamoja nasi. Roho Mtakatifu hutusaidia tuhisi upendo wa Mungu, faraja, na amani. Yeye pia hutusaidia tuhisi kusamehewa tunapotubu.

Unaweza kujifunza zaidi kuhusu agano lako la ubatizo kwa kusikiliza sala za sakramenti kila wiki (ona Mafundisho na Maagano 20:77, 79).